HOTUBA YA MHESHIMIWA *KAPT (MST)* GEORGE H. MKUCHIKA (MB), WAZIRI WA NCHI OFISI YA RAIS MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA WAKATI WA UFUNGUZI WA JENGO LA TAKUKURU WILAYA YA NGORONGORO, ARUSHA 04 SEPTEMBA 2020

Bibi Sabina Seja, Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa na Mwakilishi wa Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU**;**

Mhe. Rashid Taka, Mkuu wa Wilaya ya Ngorongoro**;**

Viongozi wa CCM Wilaya ya Ngorongoro;

Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya;

Wakuu wa Idara na Taasisi za Umma na Binafsi Mliopo;

Watumishi na Viongozi wa TAKUKURU mliopo hapa,

Viongozi wa Dini

Wageni Waalikwa,

Mabibi na Mabwana.

Habari za asubuhi.

Ndugu wageni waalikwa, napenda nitumie fursa hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya na kwa kutuwezesha kujumuika pamoja katika tukio hili la kufungua jengo la Ofisi ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) hapa Wilaya ya Ngorongoro, mkoani Arusha.

Pili, sina budi kumshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambaye ilimpendeza kuniteua nije kufungua jengo hili kwa niaba yake. Namshukuru sana.

Ikumbukwe kuwa awali, ilikuwa jengo hili lifunguliwe kwa pamoja na majengo mengine sita na Mhe. Rais Dkt. Magufuli siku ya tarehe 22 Julai 2020 alipofungua jengo la Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Chamwino, mkoani Dodoma.

Tatu, nawashukuru wageni waalikwa wote mlioweza kujumuika nasi hapa kushuhudia ufunguzi wa jengo hili la Ofisi yetu muhimu ya TAKUKURU hapa wilayani Ngorongoro. Ni dhahiri mna shughuli nyingi za maendeleo ambazo mngekuwa mnatekeleza muda huu lakini mmeona ni vema na muhimu pia kushiriki tukio hili.

Ninawashukuru sana na niwasihi ushirikiano huu usiishie leo kwa kufungua jengo hili na kuondoka, ***hapana***; tuitumie vizuri zaidi Ofisi hii ya TAKUKURU ili kwa pamoja tushiriki kuijenga Ngorongoro na Tanzania kwa ujumla kwa kuzuia na kupambana na rushwa. ***Tuwafichue wala rushwa na tuache kushiriki vitendo vya rushwa, hii ndiyo njia maridhawa kufikia maendeleo zaidi nchini.***

Ndugu wageni waalikwa,
Serikali ya awamu ya tano inayoongozwa na Jemedari na Rais wetu mpendwa, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli imefanya kazi kubwa kuimarisha na kuendeleza mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi nchini. Mimi kwa nafasi yangu ya Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora, si kwa madhumuni ya kujisifia, bali kwa madhumuni ya kueleza ukweli ni shuhuda mzuri wa hatua kubwa tuliyopiga katika mapambano dhidi ya rushwa. Tena ukweli huu siyo tu kwamba tunausemea sisi katika Serikali bali unasemwa hata na Taasisi na watu walio nje ya Serikali na nje ya Tanzania.

Ndugu wageni waalikwa,
Ripoti ya Benki ya Dunia (World Bank) ya Septemba 26, 2019 imeeleza kuwa Tanzania imeongoza kwa kupunguza umaskini miongoni mwa nchi za Afrika Kusini mwa Jangwa la Sahara. Ripoti nyingine ya Benki ya Dunia inayoitwa "*Human Capital; The Real Wealth of Nations*" iliyotoka Julai, 2019 ilionesha kuwa umaskini nchini Tanzania umepungua kutoka asilimia 34.4 hadi asilimia 26.8.

Ufanisi wa jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa nchini kwa mwaka 2018/19 zimeendelea kuonekana pia kupitia taarifa za utafiti wa kupima hali ya rushwa Duniani unaofanywa na wadau wa mapambano dhidi ya rushwa na Utawala Bora kama vile taasisi za

Transparency International (TI), MO Ibrahim na Afrobarometer. Taarifa za Taasisi hizi karibuni zinaonyesha kuwa kwa miaka mitatu mfululizo tangu mwaka 2016 hadi 2018 Tanzania imeendelea kufanya vyema katika mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora. Taasisi hizi kama nilivyosema mara kwa mara, siyo wajomba, ndugu au jamaa zetu, ni Taasisi zinazoendesha shughuli zao kwa uhuru na matokeo ya tafiti au taarifa zao yanaheshimika sana duniani.

Ndugu wageni waalikwa,

Sote tunatambua kuwa mojawapo ya madhara ya rushwa ni kuongeza umaskini katika nchi. Matokeo ya ripoti za wadau hawa yanathibitisha kuwa rushwa imepungua hapa nchini jambo linalotokana na jitihada za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa. Hivyo, kwa niaba ya Rais wetu Jemedari shupavu katika mapambano dhidi ya rushwa Mhe. Dkt. Magufuli, sina budi pia kuungana na viongozi wenzangu Serikalini kuipongeza TAKUKURU kwa kuongoza vizuri mapambano haya. Mmedhihirisha kuwa nyie ni '***mkono unaostahili kuendelea kutegemewa na Rais'*** kuongoza mapambano dhidi ya rushwa. Mmetupa heshima kubwa Wizarani lakini pia mmeipa heshima kubwa Tanzania katika uso wa ulimwengu. Hongereni sana.

Ndugu wageni waalikwa; Kwa kuthibitisha kazi nzuri TAKUKURU inayoendelea kufanya, ningependa kupongeza TAKUKURU Mkoa wa Arusha kwa kuokoa fedha kiasi cha Bilioni **2,490,396,226.00** ikiwa ni mafanikio kwa kipindi kwa mwaka 2019/2020. Kama mnavyofahamu mtazamo wa mataifa kwa sasa ni kurejesha mali zilizopatikana kwa njia ya rushwa na ubadhirifu ili zirudishwe Serikalini kwa shughuli za maendeleo.

Ndugu wageni waalikwa,

Tukio la leo la kufungua jengo la Ofisi hii ya TAKUKURU Wilaya ya Ngorongoro ni ushuhuda zaidi wa jinsi Serikali ilivyodhamiria kuendelea kuimarisha mapambano dhidi ya rushwa kwa kuijengea uwezo zaidi wa kiutendaji TAKUKURU. Nichukue fursa hii kuwapa salaam za Rais Dkt. Magufuli kuwa ataendelea kukiimarisha chombo hiki na anawataka muongeze juhudi katika kutekeleza jukumu lenu la kuzuia na kupambana na rushwa huku mkifahamu kuwa uongozi mzima wa juu kabisa wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania uko pamoja nanyi. **Chepeni kazi kwa bidii, kwani HAPA NI KAZI tu; na jengo hili liwe chachu zaidi katika utekelezaji wa majukumu yenu.**

Ndugu wageni waalikwa,

Nina imani kubwa na TAKUKURU; na nina amini kuwa hamtatuangusha sisi wasimamizi wenu katika utekelezaji wa majukumu yenu hasa pale Wizarani. Endeleeni kuhakikisha wananchi wanapata haki wanazostahili popote pale wanapoenda kupata huduma na ili pale wanaponyang'anywa na mtu au taasisi yoyote kwa njia za rushwa, TAKUKURU iwe kimbilio lao kwa sababu wanajua mtawasaidia. ***Nawasihi endeleeni kuwang'ata wala rushwa na mafisadi wote ili mradi msimuonee au kumpendelea yeyote. Endeleeni kuifanya HAKI nguzo ya utendaji wa kazi wenu wa kila siku.***

Ndugu wageni waalikwa,

Nami pia niungane pia na Rais wetu na Jemedari Mkuu wa mapambano dhidi ya rushwa, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na viongozi wengine kuwashauri watanzania wenzangu kujiepusha na vitendo vya rushwa kwa maendeleo ya Taifa. Na ili tufanikishe mapambano haya, tuanze kwa kuchagua viongozi wasiojihusisha na rushwa.

Pia niwasihi wananchi na hasa wapiga kura kutorubuniwa kwa rushwa katika uchaguzi; msiombe rushwa wala msipokee rushwa ili kumchagua mgombea au chama fulani. ***Uchaguzi usiogubikwa na vitendo vya rushwa ni moja ya viashiria muhimu vya utawala bora katika nchi. Tudhihirishe hili katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu 2020 kwa kuwakataa wote wanaotumia rushwa ili kupata uongozi.***

Ndugu wageni waalikwa,

Baada ya kusema hayo, naomba kutamka kwamba sasa nipo tayari kulifungua rasmi **JENGO LA OFISI YA TAKUKURU WILAYA YA NGORONGORO, MKOANI ARUSHA.**

ASANTENI SANA KWA KUNISIKILIZA.